


MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022)



Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022)

Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2021 – Aprili, 2022)

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyoko kusini mwa mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

a) Mwelekeo wa mvua za *Msimu* kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:

- (i) Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya na Iringa. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa mkoa wa Morogoro.
- (ii) Vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kati ya mwezi Novemba, 2021 na Januari, 2022. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa mwezi Machi 2022.
- (iii) Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika maeneo mengi na kuisha kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

b) Athari na ushauri

- (i) Upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu na kuathiri ukuaji wa mazao.
- (ii) Kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.
- (iii) Mlipuko wa magojwa unatarajiwa kujitokeza kutokana na upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama.

1. MWENENDO WA MVUA ZA VULI, 2021 NA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU NOVEMBA, 2021 HADI APRILI, 2022 (NDJFMA 2021-2022)

1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2021

Msimu wa Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba 2021 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) unatarajiwa kuendelea kama ilivyotabiriwa mwezi Septemba, 2021, ambapo maeneo mengi yalitarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani. Aidha, mvua za nje ya msimu zinatarijiwa katika mwezi Januari na Februari, 2022.

1.2 Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022)

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarijiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya na Iringa. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarijiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na kusini mwa Morogoro. Katika nusu ya kwanza ya msimu (Novemba - Januari) vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa mwezi Machi, 2022 katika nusu ya pili ya msimu. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

i. Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarijiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi. Mvua hizo zinatarijiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika maeneo mengi. Mvua hizo zinatarijiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022 katika mkoa wa Katavi na wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022 katika maeneo mengine yaliyosalia.

ii. Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Mvua katika maeneo haya zinatarijiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zinatarijiwa kuanza kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Disemba, 2021. Mvua zinatarijiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.


iii. Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarijiwa katika maeneo ya mikoa ya Rukwa, Iringa, Songwe na Mbeya. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarijiwa katika

mikoa ya Njombe, kusini mwa Morogoro na maeneo ya miinuko ya mkoa wa Mbeya. Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021 na kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022. Hata hivyo, maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021 na kuisha wiki ya kwanza ya mwezi Aprili, 2022.

iv. Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma): Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021 katika mikoa ya Lindi na Mtwara na wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021 katika mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Machi, 2022 katika mkoa wa Ruvuma na wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022 katika mikoa ya Lindi na Mtwara.

Aidha, upo uwezekano wa kutokea kwa mgandamizo mdogo wa hewa kaskazini mashariki mwa kisiwa cha Madagascar, hivyo kusababisha kurejea kwa mvua katika baadhi ya maeneo mwishoni mwa mwezi, Aprili, 2022.



Ramani 1: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 –Aprili, 2022) na Kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za Msimu (1981 -2010).

Angalizo 1: Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.

Angalizo 2: Mwelekeo wa mvua ulitolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya sasa ya joto la bahari katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki iko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika nusu ya kwanza ya msimu ingawa inaonesha kuongezeka kidogo hasa katika nusu ya pili ya msimu. Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi hususan magharibi, kusini na kanda ya kati.

Joto la bahari la mashariki mwa Bahari ya Hindi (Indonesia) linatarajiwa kuwa juu ya wastani ukilinganisha na eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki). Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na yale ya kati mwa nchi ambapo upepo wa pwani utavuma kutoka magharibi kuelekea mashariki (off-shore).

Vilevile, joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu, na juu kidogo ya wastani katika nusu ya pili ya msimu. Hali hiyo inatarajiwa kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuchelewesha mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya kusini mwa nchi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu.

Katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na Pwani ya Angola), joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu katika mifumo inayosababisha mvua kutokea katika misitu ya Kongo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

3. ATHARI NA USHAURI

Kipengele hiki cha athari na ushauri kimeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 21 Oktoba, 2021.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Kutokana na mvua za chini ya wastani hadi wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu, upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo unaweza kujitokeza. Hali hii inaweza kuathiri ukuaji wa mazao. Aidha, ongezeko la visumbufu vya mazao kama mchwa, viwavijeshi, panya na magonjwa vinatarajiwa kujitokeza katika msimu na hivyo kuathiri mazao na uzalishaji kwa ujumla. Hali kadhalika uzalishaji wa asali unatarajiwa kuathirika kutokana na upungufu wa maji na maua.

Wakulima wanashauriwa kupanda mazao na mbegu zinazokomaa ndani ya muda mfupi na zinazostahimili mvua chache kama vile mazao jamii ya mizizi na mazao ya bustani. Aidha, wanashauriwa kutumia mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo. Wakulima wazingatie kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani juu ya namna bora ya kuendesha kilimo kwa usalama wa chakula na lishe.

Mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu na ushauri kwa wakulima juu ya njia bora na namna ya kutumia kiwango kidogo cha mvua kinachotarajiwa pamoja na matumizi mazuri ya akiba ya chakula kilichopo.

b) Mifugo na Uvuvi

Upungufu wa mvua katika msimu unatarajiwa kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na kupelekea uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, baadhi ya magonjwa ya mifugo (yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao), uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo unatarajiwa kupungua. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa chakula kwa ajili ya samaki unatarajiwa kupungua na kuathiri mazao ya samaki. Hali ya ongezeko la joto inaweza kujitokeza na kusababisha vimelea vya magonjwa mbalimbali ya samaki. Kwa upande mwingine kilimo cha mwani katika maji ya kina kifupi kinatarajiwa kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu vinavyotarajiwa.

Jamii inashauriwa kuweka mpango mzuri wa matumizi na uhifadhi wa maji na malisho, kufuga kibiashara na kuvuna mifugo kulingana na upatikanaji wa malisho na maji. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa watumie taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani. Aidha, Wakulima wa mwani katika Mikoa ya Lindi na Mtwara wanashauriwa kupanda aina ya mbegu zinazostawi kwenye maji ya kina kirefu.

c) Utalii na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji kwa wanyamapori inatarajiwa kupungua kutokana na mtawanyiko hafifu wa mvua unaotarajiwa. Hali hii inaweza kusababisha migogoro baina ya wanyamapori na jamii inayozunguka hifadhi za wanyamapori. Aidha, kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko kwa wanyama wanaofugwa na wanyamapori kunaweza kujitokeza kutokana na mwingiliano wakati wa kutafuta maji na malisho.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya usafirishaji katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii pamoja na kuchukua hatua stahiki. Aidha, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa Mamlaka husika pindi kunapokua na uvamizi wa wanyamapori katika makazi.

d) Usafiri na Usafirishaji

Maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, hivyo sekta ya usafiri na usafirishaji hususan usafiri wa ardhini, anga na kwenye maji zinaweza kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyoweza kujitokeza. Aidha, shughuli za uendeshaji wa meli na miundombinu katika bandari inatarajiwa kunufaika katika kipindi cha msimu huu. Hata hivyo, inashauriwa kuwa mipango ya utekelezaji na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya sekta ya uchukuzi izingatie taarifa za utabiri wa hali ya hewa katika eneo husika.

e) Nishati, Maji na Madini

Kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani. Hali hii inaweza kupunguza upatikanaji wa maji kwa matumizi mbalimbali na kupelekea migogoro baina ya watumiaji wakubwa na wadogo. Katika sekta ya madini, uzalishaji wa madini (hususan dhahabu kwa wachimbaji wadogo) unaweza kuongezeka kutokana na upungufu wa mvua unaotarajiwa. Kwa upande mwingine, wachimbaji wenye matumizi makubwa ya maji uzalishaji unaweza kuathirika. Uzalishaji wa nishati ya umeme utokanao na maji unaweza kuathirika. Hata hivyo, utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya umeme, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi unatarajiwa kuendelea vizuri.

Wadau wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji katika shughuli za kuchakata madini, uzalishaji wa umeme, matumizi viwandani na majumbani. Vilevile, Sekta ziendeele kufuatilia tabiri zitolewazo na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

f) Mamlaka za Miji

Kutokana na matarajio ya upungufu wa mvua, mamlaka za miji zinashauriwa kutumia fursa hiyo kuweka miundombinu bora kama majengo, maghala, sehemu za kuhifadha taka, umeme, pamoja na kuhakikisha kuwa mifumo ya utiririshaji maji inafanya kazi katika kiwango kinachostahili. Mamlaka hizo zinashauriwa kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa ili kudhibiti upotevu wa maji na pia kusimamia matumizi endelevu ya maji. Mamlaka za Miji pia zinashauriwa kuandaa programu za kuhimiza kilimo cha mazao yanayostahimili mvua chache ili kuboresha upatikanaji wa chakula.

g) Sekta ya Afya

Kwa maeneo yanayotarajia kupata mvua za chini ya wastani, upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama unaweza kujitokeza na kupelekea mlipuko wa magojwa. Mamlaka za afya zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kuvuna na kutibu maji kabla ya kutumia.

Kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani, pamoja na hatua zilizoelezwa hapo juu, wananchi wanashauriwa kuharibu mazalia ya wadudu wadhurifu kama vile mbu. Msisitizo unatolewa kwa mamlaka husika kutoa elimu ya afya kwa wananchi na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

h) Sekta Binafsi

Kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, shughuli za kiuchumi kama vile uzalishaji na uhifadhi wa mazao tete na bidhaa zinaweza kuathirika kutokana na kuongezeka kwa gharama. Vilevile, mvua za chini ya wastani zinaweza kusababisha ubora wa miti ya nguzo na mbao kuathirika.

Sekta binafsi inashauriwa kushirikiana na wataalamu wa sekta mbalimbali katika kutoa elimu pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuimarisha uwekezaji na kulinda mitaji ya kibiashara.

i) Menejimenti za Maafa

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, madhara yanayoweza kujitokeza ni pamoja na upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula, malisho ya mifugo na maji. Mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayohamasisha uhifadhi wa chakula, maji na malisho ya mifugo.

j) Vyombo vya habari

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa mvua za Msimu pamoja na taarifa zilizo huishwa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa watoa taarifa wa sekta mbalimbali zinazotumia taarifa za hali ya hewa. Pia kuandaa na kusambaza makala na taarifa za tahadhari za kisekta kwa kutumia lugha nyepesi kwa lengo la kuhabarisha na kuelimisha jamii ipasavyo juu ya matumizi ya utabiri wa hali ya hewa katika kupunguza athari za hali mbaya ya hewa.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa: 27 Oktoba, 2021

Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania